

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YA HUDUMA ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA MPANDA (“MPANDA WSSA”) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

OMBI LA MAPITIO YA BEI NAMBA: TR-W-18-055

Mnamo tarehe 20 Mei 2019, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Mpanda (Mpanda WSSA) la kutaka kurekebisha bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Jedwali namba 1 hadi 4 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa kwa wateja wenye Dira (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei zinazopendekezwa			
		2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani					
Band 1 (0-10)	950	1,200	1,300	1,300	
Band 2(11-20)	950	1,600	1,800	1,800	
Band 3 (21 na zaidi)	950	1,700	1,800	1,800	
Taasisi	1020	1,700	1,790	1,810	
Biashara	1050	1,700	1,840	1,860	
Viwandani	1200	1,930	2,100	2,130	
Magati	1000	1,000	1,000	1,000	

Jedwali 2: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa kwa wateja wasio na Dira(Shilingi/mwezi)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei zilizopendekezwa			
		2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	14,000	26,400	Mpanda itahakikisha kuwa wateja wote wanafungiwa Dira		
Taasisi			Wateja wote wa makundi haya wamefungiwa Dira		
Biashara					
Viwandani					
Magati					

Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Kundi la Wateja	Tozo za Sasa	Tozo zilizopendekezwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani				
Taasisi	Asilimia 20 ya gharama ya vifaa, kwa mujibu wa sehemu ya 24 ya Kanuni za Majisafi na usafi wa Mazingira za mwaka 2013			
Biashara				
Viwandani				
Magati				

Jedwali 4: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)

Kundi la Wateja	Tozo za Sasa	Tozo zilizopendekezwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	15,000	25,800	26,728	27,691
Taasisi	15,000	48,000	49,728	51,518
Biashara	15,000	48,000	49,728	51,518
Viwandani	15,000	373,200	386,635	400,554
Magati	15,000	48,000	49,728	51,518

Kwa mujibu wa wasilisho la Mpanda WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kupata mapato ili kumudu gharama halisi za uendeshaji. Mamlaka ya maji Mpanda wamebainisha kuwa mabadiliko ya bei na tozo yanayopendekezwa yataiwezesha kuongeza mtandao wa majisafi na kufanya uwekezaji wa miundombinu ya maji ili kuboresha utoaji wa huduma ya maji safi katika mji wa Mpanda.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumanne, tarehe 23 Julai 2019, katika Ukumbi wa Polisi Club, Mjini Mpanda** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **30 Julai 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana **OFISI ZA EWURA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI, GHOROFA YA SITA, JENGO LA NHIF, MTAA WA KARUME, S.L.P 2245 MBEYA** au **OFISI ZA MAMILAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MPANDA**.

Imetolewa na:

Kaimu Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

28 Juni 2019